**BARAZA LA WAKUU WA SHULE ZA KIISLAMU TANZANIA**

**MUONGOZO WA USAHIHISHAJI WA MTIHANI WA UTAMILIFU WA SHULE ZA KIISLAMU KIDATO SITA**

**2025 – KISWAHILI 1**

**121/1** **2025**

**SEHEMU A : Alama 40**

1. Mtahiniwa anapaswa kusoma Habari aliyopewa kisha kujibu maswali aliyopewa.

(a) Kichwa cha Habari hiyo kinaweza kuwa
ATHARI YA UTUMIAJI MIHADHARATI
MADHARA YA UTUMIAJI WA MIHADHARATI
MAISHA YA MACHUPA NA DIMOSO
MAISHA YA MACHUPA
Na vingine visivyokuwa hivyo vinavyoendana na Habari mtahiniwa apewe alama. (Kichwa cha Habari lazima kiandikwe kwa herufi kubwa)

(b) Methali zinazofanana na Habari hiyo ni
(i) Pema unapo pema, ukipema si pema tena.
(ii) Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu. Mdharau mwiba mguu huota tende.
(iii) Sikio la kufa halisikii dawa.
(Na nyingine zinazoendana na swal mtahiniwa apewe alama).
**[Alama 01 @ kipengele**

(c) Vijana wengi hujikuta wakiangukia katika dimbwi la utumiaji mihadharati kwa sababu mbalimbali kama vile:
(i) Kudhani kwamba ndiyo kwenda na wakati au mtindo mpya wa Maisha.
(ii) Kujiliwaza au kupunguza msongo wa Mawazo.
(Na nyingine zisizokuwa apewe alama)
**Alama 01 @ kipengele**

(d) Athari za utumiaji wa mihadharati ni kama zifuatazo:
(i) Kukithiri vitendo vya uvunjifu wa amani kama vile ujambazi na unyang' anyi.
(ii) Kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza kama vile UKIMWI.
(Na nyingine zisizokuwa hizo apewe alama)
**Alama 01 @ kipengele**

(e) Namna bora ya kuisaidia serikali kuepukana na janga hili ni:
(i) Kutoa taarifa kwa vyombo vya serikali kama vile Polisi haraka iwezekanavhyo mara tu unapohisi ama kuona makundi ya watumiaji mihadharati.
(ii) Kuelimisha jamii juu ya madhara yatokanayo na utumiaji wa mihadharati.

(Na nyingine zisizokuwa hizo mtahiniwa apewe alama)
**Alama 01 @ kipengele**

2. Mtahiniwa anapaswa kueleza udhaifu wa mtazamo wa kimapokeo (kimofilojia) katika kuainisha ngeli za nomino.
   (i) Baadhi ya nomino hazina maumbo ya umoja na wingi. Mf. Kalamu, karatasi n.k
   (ii) Uanishaji wa ngeli ya 16, 17 na 18 unajikita katika vielezi vya mahali na si katika nomino.
   (iii) Kuna baadhi ya mwingiliano wa viambishi katika baadhi ya ngeli. Mf. Viambishi vya ngeli ya kwanza umoja vinafanana na vya ngeli ya tatu umoja.
   (iv) Wanaisimu walioanisha mtazamo hu wametafautiana katika idadi ya ngeli, mf. Guthrie na Palome 18 wakati Broomfield 8 tu.
   (v) Nomino za viumbe hai zimechanganywa na viumbe visivyo hai katika ngeli ya ki-vi Mf. Kiti-viti, kiongozi – viongozi.
   (Na nyingine zisizokuwa hizo apewe alama)
   **Alama 02 @ kipengele**

3. Mtahiniwa anapaswa kueleza miundo tofautitofauti ya kirai (KN) kwa kutoa mifano.
   (i) Nomino moja pekee. Mf. <u>Mwanamichezo</u> amependeza
   <u>Mtoto</u> anacheza vizuri
   (ii) Nomino mbili au zaidi zilizounganishwa na kiunganishi.
   Mf. <u>Baba na mama</u> wanakula.
   <u>Juma, Fatma na Iddi</u> ni wanafunzi
   (iii) Kiwakilishi kimoja au zaidi
   Mf. <u>Sisi</u> tulimuona. <u>Mimi na wewe</u> hatukumuona.
   (iv) Kiwakilishi na kivumishi, Mf. <u>Sisi sote</u> ni ndugu. <u>Kile kibaya</u> kimepotea
   (v) Nomino na kishazi rejeshi. Mf.
   Wanafunzi waliokuja jana wamechoka.
   <u>Kalamu iliyopotea</u> imeonekana

   (vi) Nomino na kivumishi kimoja au zaidi
   Mf. <u>Mtoto mzuri</u> anakula
   <u>Magari makubwa mabovu</u> yamegongana
   (Na miundo mengine isiyokuwa hiyo apewe alama.
   **Alama 02 @ kipengele**

4. Mtahiniwa anapaswa kueleza changamoto ya kutumia misimu katika lugha.
   (i) Mara nyingi huongeza chumvi inapotumika katika mawasiliano.
   (ii) Kupoteza maana wakati wa kuwasiliana savbabu hutumiwa na kundi la watu maalumu hivyo wengine ni vigumu kuelewa kinachomaanishwa.
   (iii) Misimu ina sifa ya kuwa na maana zaidi ya moja. Mf. Kula kichwa, kwa muktadha wa daladala maana yake chukua abiria ila muktadha wa chuoni maana ni kufeli kimasomo.
   (iv) Kumchanganya mtumiaji mgeni wa lugha poale anapooanza kujifunza. Sababu hutumia lugha ya mafumbo. Mf. Kuupiga mwingi.

(v) Misimu huweza kuleta migogoro baina ya wanazungumzaji pale lugha ya kejeli inapotumika. Mf. Chawa achene mambo yenu".
(Na nyingine zisizokuwa hizo apewe alama)
**Alama 02 kila kipengele**

**SEHEMU B (Alama 60)**

5. Mtahiniwa anapaswa kuleza sifa za matangazo na pia kiandika tangazo kutokana na maelekezo ya swali husika.
(a) Tangazo linapaswa kuwa na sifa zifuatazo:
   (i) Kichwa cha tangazo
   (ii) Cheo /jina la mtoa tangazo
   (iii) Lugha nyepesi na yenye kueleweka kwa urahisi
   (iv) Matumizi ya michoro na picha zenye mvuto kwa walengwa
   (v) Kueleza jambo kwa ufupi
   (vi) Ubunifu katika uwasilishaji
   Na zinazofanana na hizo. **@ 02 = Alama 10**

(b) Mtahiniwa anapaswa kuandika tangazo kwa kuzingatia yafuatayo:
   (i) Kichwa cha tangazo
   (ii) Wahusika au mhusika wa tangazo
   (iii) Sababu au lengo la tangazo
   (iv) Mahali, muda, mawasiliano au anuani
   (v) Cheo au wadhifa wa aliyetoa tangazo
   **@ 02 = alama 10**
   **[Jumla alama 20]**

6. Swali linamtaka mtahiniwa kueleza mchango wa mashirika ya dini katika kukuza na kueneza Kiswahili nchini Tanganyika wakati wa utawala wa Waingereza.

Utangulizi: **Alama 2.5**
Maelezo mafupi kuhusu maendeleo ya Kiswahili wakati wa utawala wa Waingereza/kukuana kuenea kwa Kiswahili enzi za Waingereza.

Kiini **(Alama 15)**
(i) Kutafsiri maandiko kwa lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, Biblia na vitabu vya nyimbo.
(ii) Kuandaa machapisho kwa lugha ya Kiswahili. Mfano, Mwaka 1905 misheni ya Magila Muheza, Tanga ilitoa kitabu cha Habari za Wakilindi kilichoeleza Habari za Wasambaa.
(iii) Kuandaa na kuandika kamusi ya Kiswahili. Kiingereza na Kiingereza, Kiingereza na Kiswahili. Mf. Shirika la SPCK iliyoandikwa na Askofu Edward Steer na kukamilishwa na A. Madan.
(iv) Kuchapisha magazeti ya Kiswahili. Kwa mfano shirika la UMCA liliandika magazeti ya Barazani na Rafiki Yangu (1910).

(v) Kutoa huduma ya Elimu kwa jamii. Kwa mfano walijenga shule mbalimbali kama vile Magila, Ndanda, Kigonsela n.k. ambapo lugha ya Kiswahili ilitumika kutolea elimu na pia kama somo.

(vi) Walitumia lugha ya Kiswahili kihubiri dini na nyinginezo. @ **3 = 15**

**HITIMISHO**

Maelezo mafupi kuhusu mchango wa mashirika haya katika kukuza lugha ya Kiswahili nchini Tanganyika.

Na nyinginezo @ **03 = alama 15**

7. Mtahiniwa anapaswa kueleza kinagaubaga changamoto zinazoikabili lugha ya Kiswahili ulimwenguni kwa sasa

Utangulizi **Alama 2.5**

Maelezo mafupi kuhusu lugha ya Kiswahili.

**Kiini**

Kuelezea changamoto hizo kwa mifano:

(i) Kutopewa hadhi ya kutumika katika baadhi ya maeneo. Mfano Mikutano mingi ya kimataifa.

(ii) Matumizi ya istilahi za kigeni wakati uzungumzaji wa Kiswahili.

(iii) Ufinyu wa bajeti, kuwezesha asasi na taasisi zinazosimamia maendeleo ya Kiswahili kama vile CHAUKIDU, CHAKA, TUKI na BAKITA.

(iv) Usambazaji duni wa taarifa na machapisho ya Kiswahili ulimwenguni.

(v) Uhaba wa wakufunzi wa lugha ya Kiswahili.

Na nyinginezo @ **03 = alama 15**

**Hitimsho** **Alama 2.5**

**JUMLA ALAMA 20**

8. Mtahini anatakiwa kuelezea kwa kina zana muhimu zinazohitajika katika suala zima la ukalimani.

Utangulizi **Alama 2.5**

Maelezo mafupi kuhusu ukalimani na zana za ukalimani.

Kiini

Maelezo ya kina kuhusu zana hizo.

(i) Kitururu: Chumba maalumu ambacho hutumiwa na mkalimani.

(ii) Panel: Pokezi na tolezi ya sauti.

Hutumika kupokea sauti chanzi na kutolea sauti ya mkalimani wakati wa zoezi la ukalimani.

(iii) Maikrofoni

Hutumika na mkalimani wakati wa kuongea.

(iv) Kompyuta
Hutumika na mkalimani

(v)